

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA - MIKINDANI



Tarehe: **09/11/2021**

YAH: TANGAZO LA ZABUNI

Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara - Mikindani kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 inatarajia kutekeleza Miradi mbalimbali ya Maendeleo yenye thamani ya shilingi za kitanzania **11,647,818,027.89**. Miradi hiyo imegawanyika katika sekta za Afya, Elimu Msingi, Elimu Sekondari Majengo - Ujenzi, Maendeleo ya Jamii, Mipango Miji na sekta ya Utawala.

1. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani anakaribisha maombi ya Mafundi wenyeji (Local fundi), Taasisi za Kiserikari au vikundi vya ujenzi wa majengo wenye sifa zifuatazo: -

- Awe na cheti cha ufundi kutoka chuo cha ufundi kinachotambulika na Serikali.
- Awe tayari kuheshimu mkataba wa kazi atakayopewa.
- Awe anajua kusoma michoro na ramani ya nyumba.
- Awe na uwezo ,nguvu kazi ya kutosha ,uzofu wa kazi wa kujenga majengo ya serikari na vitendea kazi.
- Awe na Akaunti ya benki kwa ajili ya malipo ya kibenki kwa malipo ya kazi atakazokuwa anazifanya.
- Fundi awe na uwezo wa kujenga, kumaliza na kukabidhi kwa Muda atakaopangiwa.


ZINGATIO:

- Nguvu ya kisheria (Power of Attorney) ni kwa Taasisi za kiserikari au vikundi vilivyosajiliwa kisheria.
- Maombi yaambatanishwe na nakala ya vyeti vya ufundi na wasifu binasfi wa kazi
- Maombi yafungwe kwenye bahasha ya khaki (A4) yenye lakiri iandikwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Manispaa,
Mtwara - Mikindani,
S.L.P 92,
MTWARA.

- Maombi yawasilishwe katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya zabuni Kitengo cha Manunuzi Makao Makuu ya Manispaa.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15/01/2021 saa 5:00 asubuhi na ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea maombi na wawakilishi watakaoamua kuhudhuria ufunguzi huo wanakaribishwa.


COL. Emanuel H. Mwaigobeko
MKURUGENZI WA MANISPAA
MTWARA - MIKINDANI

MKURUGENZI WA MANISPAA
MTWARA - MIKINDANI
S. L. P. 92
MTWARA